HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA
SHULE YA SEKONDARI KIWANJA

S.L.P 178,
CHUNYA

KUMB.NA KJSS/JI/2021/VOL. IV/03 07/12/2021

Mzazi wa.....,
S.L.P.....
CHUNYA

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA (HOSTELI) KIWANJA SEKONDARI 2021.

1.0 UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza Kiwanja sekondari mwaka **2021**. Shule ya sekondari Kiwanja ipo umbali wa km 3 kutoka makao makuu ya halmashauri ya Wilaya ya Chunya. Shule ni ya hosteli kwa wanafunzi wote wa kidato cha kwanza hadi cha nne na bweni kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita.
Muhula wa kwanza kwa mwaka 2021 utaanza rasmi tarehe **11.01.2021**. Mwanao anatakiwa kufika shuleni tarehe **10.01.2021** kwa ajili ya kuanza mafunzo ya awali yaani orientation course tarehe **11.01.2021**. Ni muhimu wewe kama mzazi kukumbuka kuwa ikiwa mwanao hatafika baada ya majuma mawili toka tarehe ya kufungua shule yaani tarehe 23/01/2021 nafasi yake atapewa mtu mwingine mwenye uhitaji wa hosteli.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

Serikali inatoa elimu bila malipo kwa wanafunzi wote wa kidato cha kwanza hadi cha nne. Hivyo wewe kama mzazi unatakiwa kuunga mkono juhudi hizi za serikali kwa kumnunulia mwanao mahitaji yote muhimu kama vile sare, madaftari,magodoro na kumlipia gharama za chakula awepo shuleni pamoja na nauli ya kwenda na kurudi shuleni.

2.1 Sare za shule

(i) Wavulana.

(a) Suruali mbili, moja rangi ya kijani kibichi na nyingine rangi ya ugoro. Mshono wa suruali ni turn up na chini iwe na upana wa kutosha kuingia chupa ya soda.
(b) Shati nyeupe mbili Mikono mifupi.

(c) sare za michezo ni T- Shirt moja blue yenye nembo ya shule, Tracksuit moja rangi ya blue na bukta ya blue.
(d) Sweta mbili moja rangi ya kijani kibichi na nyingine rangi ya ugoro.
(e) Viatu vyeusi jozi mbili vya kamba vyenye kisigino kifupi.
(f) Soksi nyeusi jozi mbili
(g) Mkanda mweusi

(ii) Wasichana

(a) Sketi mbili, moja rangi ya kijani kibichi na nyingine rangi ya ugoro. Mshono wa Sketi ni linda za kawaida na iwe ndefu sana.
(b) Blauzi nyeupe mbili Mikono mifupi.
(c) sare za michezo ni T- Shirt moja blue yenye nembo ya shule, Tracksuit moja rangi ya nyeusi
(d) Sweta mbili moja rangi ya kijani kibichi na nyingine rangi ya ugoro.
(e) Viatu vyeusi jozi mbili vya kamba vyenye kisigino kifupi.
(f) Soksi nyeupe jozi mbili
(g) Hijabu nyeupe kwa waislamu.

2.2 Nguo za kushindia (Shamba dress), vifaa chakula/darasani, godoro, nk.

Wanafunzi muda wote na katika maisha yao yote ya shuleni kamwe wasije na nguo ambazo hazijaruhusiwa. Wanafunzi wanatakiwa kuja na nguo zifuatazo kwa ajili ya kuvaa nyakati ambazo si za masomo.

(i) Suruali mbili nyeusi kwa wavulana na sketi mbili nyeusi kwa wasichana. Mshono uwe sawa na ule wa sare za shule.
(ii) T- Shirt moja ya blue yenye nembo ya shule kwa wote
(iii) Kanga moja kwa wasichana (ivaliwe akiwa bwenini tu)
(iv) Tracksuit moja blue kwa wavulana na nyeusi kwa wasichana. ***Kwa wazazi ambao hali ya uchumi si rafiki mwanafunzi anaweza kutumia tracksuit moja kwa ajili ya michezo na kama shamba dress.***
(v) Gauni refu rangi ya dark blue kwa wasichana na mshono wake uwe wa solo.
(vi) Shuka mbili moja rangi ya pink na nyingine blue.
(vii) Tranka kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake.
(viii) Nguo za ndani za kutosha
(ix) Sahani, kikombe, kijiko, ndoo ya kuogea,mswaki, sabuni za kutosha, net, mto nk.
(x) Daftari kubwa Q2 angalau kumi.
(xi) Godoro futi 2.5

2.2 GHARAMA ZA CHAKULA.

Ili kuwawezesha watoto kuishi shuleni wazazi watalazimika kuchangia vyakula. Mchanganuo wa michango ya chakula kwa muhula ni kama inavyoonesha hapa chini.

NA	AINA YA CHAKULA	KIASI KWA MIEZI MITANO
1	Unga safi wa sembe	Kilo 65
2	Maharage	Kilo 30
3	Mchele safi wa Kyela	Kilo 13
4	Nyama	Kilo 3
5	Sukari	Kilo 6
6	Mboga za majani	Kilo 3
7	Chumvi	Kilo 3
8	Mafuta ya kupikia	Lita 5
9	Vitunguu	Kilo 3
10	Nyanya	Kilo 3

Chakula kitakusanywa na kamati ya wazazi na mpishi atagharamiwa baada kuangaliwa na kamati hiyo. Aidha kuna vyakula ambavyo haviwezi kuletwa na mzazi mmojammoja kama vile nyama, mboga za majani, nyanya nk. Kamati baada ya kufungua shule hukaa na wazazi na kuangalia namna nzuri inayofaa.

3.0 BIMA ZA AFYA KWA AJILI YA WANAFUNZI.

Ili kuwawezesha wanafunzi kuishi salama na kupata matibabu pale wanapoumwa kila mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya , au wazai wanaweza kukubaliana watoto wao kuunda kaya na kupatiwa kadi baada ya kuripoti.

4.0 SHERIA ZA SHULE .

Kila mwanafunzi atatakiwa kufuata sheria za shule wakati wote akiwa shuleni. Aidha mzazi ***usimpe mwanao simu hata kama unampenda sana*** akiwa na shida atakupigia kwa namba ya shule **0755262569.** Wazazi mnahimizwa pia kutowapa wanafunzi fedha nyingi sana kwa ajili ya matumizi. Utafiti unaonyesha kuwa watoto wanaopewa fedha huanza kuhangaika na namna ya kuzitumia fedha walizopewa badala ya kusoma.

Mwisho napenda kumkaribisha sana mwanao Kiwanja sekondari.

E. J. MNYALAPE
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIWANJA
CHUNYA – MBEYA

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIWANJA
CHUNYA – MBEYA

SHULE YA SEKONDARI KIWANJA
SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE
MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 7 bila taarifa yoyote /utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.

(vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(ix) Uvutaji wa sigara.

(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.

(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni .

(XV) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au vifaa vinavyohusiana na simu..

(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa .

(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

MKUU WA SHULE
...LE YA SEKONDARI KIWANJA
CHUNYA – MBEYA

OFISI YA RAIS,

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA
SHULE YA SEKONDARI KIWANJA
FOMU YA KUKUBALI

1. Mimi .....ambaye ni Mvulana/, nimekubali kuingia kidato cha **kwanza** Katika shule ya sekondari kiwanja kama mwanafunzi wa Bweni/Hostel tarehe **10/01/2021** nitafika shuleni bila kuchelewa na kusoma kwa bidii.
2. Nitatii sheria za shule, na sitajihusisha wala kuchochea mgomo shuleni. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo, nidhamu na kazi za kujitegemea.
   Ninaahidi kuwa nitasoma na kufaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza hadi la pili ambavyo ndiyo viwango vilivyoweka na shule.
3. Sahihi ya mwanafunzi ..... Tarehe .....

SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI

1. Mimi ..... Nimekubali mtoto wangu
   ..... Asome katika shule ya sekondari Kiwanja kuanzia tarehe **10/01/2021**

2. Ninaahidi kumpa vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua.

3. Nitahakikisha kuwa ninamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea.

4. Ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari Kiwanja kama mwanafunzi wa Hosteli na ataendelea hivyo hadi atakapo maliza kidato cha nne mwaka **2024** Naelewa nafasi za kidato cha kwanza hosteli ni haba sana, hivyo mimi wala mwanangu hatutamsumbua Mkuu wa shule wala uongozi wa shule kwa vyovyote

5. Ninaahidi kumsimamia kusoma kwa bidii na kupata daraja la ***kwanza hadi la pili*** kulingana na malengo ya shule.

6. Anwani yangu ya kudumu ni:

.....

.....

Sahihi ..... Tarehe.....

Fomu hii inatakiwa kujazwa na ndugu 3 wa karibu wa mwanafunzi:

Jina la ndugu	Mahali anapoishi	Namba ya simu	Kazi

Ni vema ikakukmbukwa kuwa ndugu waliojazwa kwenye fomu ndiyo wanaoweza kumtembelea mwanafunzi akiwa shuleni

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIWANJA
CHUNYA – MBEYA

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIWANJA
CHUNYA – MBEYA

PRESDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

KIWANJA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 178
CHUNYA
Date: ...../...../ 20.....

TO MEDICAL OFFICER
.....
.....
.....

PART A

Student's name .....
Please examine the above named student to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following:

1. Haemoglobin.....
2. P.V. Bleeding.....
3. Sight.....
4. Blood pressure.....
5. Urine for sugar and pregnant test.....
6. Stool for routine examination.....
7. Asthma.....
8. Skin diseases.....
9. Leprosy.....
10. Any deformity.....
11. Epilepsy.....
12. Pulmonary tuberculosis.....
13. Neurosis.....
14. General diseases.....

PART B:
MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government medical Officer)
I have examined the above named student and consider that he/she is physically and mental fit/unfit to join the school for the year 2021.

.....
Signature (Dr)